# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA WAZIRI MKUU

# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

## SHULE YA SEKONDARI NASSA

## S.L.P 440

## BUSEGA- SIMIYU

**NAMBA YA USAJILI WA SHULE: S.786**

**NAMBA YA KITUO CHA MTIHANI: S1029**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**KUMB.NSS/F5/BDC/2026/VOL3/.........**
**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P …………………………………..**
**…………………………………………….**

YAH**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NASSA HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA MKOA WA SIMIYU MWAKA..............**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha tano katika shule hii kwa mwaka wa masomo....................na atasoma tahasusi ya ………………

## 1.0 MAHALI SHULE ILIPO

Shule ya Sekondari **NASSA** ipo Kata ya Nyashimo Wilayani Busega Mkoa wa **Simiyu.** Shule ipo umbali wa kilometa tatu hivi kutoka kituo cha mabasi Nyashimo (Nyashimo Bus Stand), barabara kuu ya kutoka Mwanza kwenda Musoma. Shule ipo upande wa kulia wa barabara ukiwa unatokea Mwanza na upande wa kushoto ukiwa unatokea Musoma au Bariadi. Shule iko barabarani na inafikika kwa urahisi kwa usafiri wa magari ya abiria kutoka Mikoa ya Dar es Salaam, Kagera, Arusha, Mwanza na Mara (Musoma)**.**

Ukiwa unatoka Dar es Salaam, Arusha, Singida, Dodoma, Mbeya, Tabora, Katavi, Shinyanga kupitia Bariadi utashukia kituo cha mabasi Lamadi. Baada ya hapo utapanda mabasi yanayotoka Musoma au Bariadi kwenda Mwanza na utamuomba kondakta akushushe shule ya Sekondari Nassa (Nauli ni shilingi elfu tatu kutoka Lamadi hadi shule ilipo). Kwa wanaotoka Mikoa ya Kagera, kigoma, watapanda mabasi ya Mwanza kuelekea Musoma na washuke kituo cha mabasi Nyashimo. Baada ya kushuka utapanda bodaboda itakayokufikisha shuleni kwa gharama ya shilingi elfu mbili.

**…………………………..**
**JAPHET SIRIKWA JOSEPH**
**MKUU WA SHULE.**
**SHULE YA SEKONDARI NASSA**

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:-

### 2.1. Sare za Shule (Wasichana)

2.1.1. Sketi mbili za rangi ya buluu - Rangi ya idara ya maji (Turchese Ral 5018). Sketi iwe ndefu inayofika kwenye kifundo cha miguu. Sketi iwe na marinda sita (mbele marinda matatu na nyuma marinda matatu ya linda box linalofunguka kuanzia kwenye belt (Angalia picha na mchoro kwenye kiambata "A" nyuma ya fomu hii)
2.1.2. Shati mbili Nyeupe zenye mikono mirefu kitambaa cha tetroni
2.1.3. Hijab (kijuba) NYEUPE inayofunika kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mguu akisimama (Hii ni kwa wanafunzi Waislamu).
2.1.4. Raba nyeupe, Track suit na T-Shirt, zote zikiwa na rangi ya damu ya mzee
2.1.5. Viatu vyeusi vya kufunga na kamba vyenye kisigino kifupi.
2.1.6. Soksi nyeupe ndefu (free size) jozi nne.
2.1.7**.** Sweta moja rangi kijani jeshi
2.1.8. Fulana Dark Blue (T-shirt) moja.
2.1.9. Gauni mbili za kushindia (Shamba dress) rangi ya light blue yenye mshono wa Solo. Gauni hizi ziwe ndefu zinazofika kwenye kifundo cha mguu. Aina ya kitambaa kiwe ni cha esteem namba moja.


**NB**. Kwa wanaovaa hijabu ya kushindia ifanane na rangi ya gauni la kushindia- shamba dress (Angalia picha na mchoro kwenye kiambata "B")



### 2.2. Sare za Shule (Wavulana)

2.2.1 Suruali mbili za rangi ya bluu - Rangi ya idara ya maji (blue turchere). Suruali iwe yenye marinda, ndefu ya kufika kwenye kifundo cha miguu na isiwe nyembamba (**modal).**
2.2.2. Mashati mawili meupe ya kitambaa cha tetroni. Mashati yawe ya mikono mirefu yanayofikia kwenye kifundo cha mikono.
2.2.3**.** Raba nyeupe, Track Suit, na T-shirt vyote vikiwa na rangi ya damu ya mzee kwa ajili ya michezo.
2.2.4. Viatu vya shule vyeusi vya kufunga na kamba vyenye kisigino kifupi

2.2.5. Soksi za shule nyeusi jozi nne
2.2.6. Fulana Dark Blue (T-shirt)
2.2.7. Sweta la rangi ya kijivu.
2.2.8 . **Nguo za kushindia**, Suruali mbili za rangi nyeusi Suruali iwe yenye marinda, ndefu ya kufika kwenye kifundo cha miguu na isiwe nyembamba (**modal)**.Pia Fulana (T-shirt) light bluu moja.



**2.3. Mahitaji ya darasani**

2.3.1. Madaftari kulingana na tahasusi aliyochaguliwa
2.3.2. Vitabu vya masomo ya darasani kutegemeana na tahasusi husika.
2.3.3. Scientific Calculator kwa wanaosoma tahasusi za HGL, HGK na HGE
2.3.4. Advanced Oxford Dictionary ($9^{th}$ Edition+)
2.3.5. Kalamu za bluu na nyeusi za kutosha
2.3.6. Penseli (HB)
2.3.7. Rula
2.3.8. Bunda (reams) mbili za karatasi aina ya **“Double A”**

**2.4. Mahitaji ya Bwenini**

2.4.1. Godoro futi mbili na nusu kwa sita
2.4.2. Mashuka Jozi 2 rangi ya pink, blanket moja, night dress, foronya ya godoro moja na chandarua.
2.4.3. Nguo za ndani za kutosha;
2.4.4. Vyombo vya chakula (sahani ya bati au plastiki, bakuli, kijiko, kikombe na galoni moja kwa ajili ya kutunzia maji safi na salama ya kunywa),
2.4.5. Ndoo mbili (moja ya lita kumi na nyingine ya lita ishirini) zenye mifuniko
2.4.6. Kwanja moja, jembe moja, mfagio mgumu (hard broom) mmoja, panga moja, mifagio (miwili, wa ndani na wa nje) pamoja na mopa moja.
2.4.7. Dawa ya chooni lita mbili na nusu (2.5Lit).

**2.5. Mahitaji mengine**

2.5.1. Namba ya mzazi ama mlezi inayopatikana whatsApp
2.5.2. Kanga/kitenge angalao pair moja
2.5.3. Taulo, kitana, mafuta ya ngozi, sabuni za kufulia na kuogea, kanda mbili (slippers), nail cutter, shaver na vibanio vya nguo.
2.5.4. Mswaki na dawa ya meno

2.5.5. Begi au sanduku la kutunzia vitu vyake
2.5.6. Begi dogo la madaftari.

### 3.0. MICHANGO MBALIMBALI

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**MICHANGO HII ILIPWE KUPITIA BANK YA NMB AKAUNTI NUMBER 3122300046 (ELIMU YA KUJITEGEMEA NASSA SEKONDARI). UNAPOLIPA MICHANGO HII, TAFADHALI HAKIKISHA JINA KAMILI LA MWANAFUNZI LINAINGIZWA KWENYE MFUMO WA BENKI NA NI MALIPO KWA AJILI YA NINI. MWANAFUNZI ATATAKIWA KUJA NA NAKALA YA PAY SLIP SIKU YA KURIPOTI SHULENI**

## 4.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

4.1. Mwanafunzi anatakiwa kuwa na adabu na heshima wakati wote. Mwanafunzi anapaswa kuheshimu watu wote kulingana na hadhi zao. Mwanafunzi anapaswa kutumia lugha ya upole wakati wote anapoongea na wengine. Kamwe lugha ya matusi haitavumiliwa shuleni. Mwanafunzi atakaetenda kosa la kutukana au kudhalilisha wengine **atafukuzwa shule**.

4.2. Mwanafunzi anapaswa kutii ratiba ya shule wakati wote. Hii ni pamoja na kujali na kutunza muda kulingana na ratiba atakayokuwa amepewa.

4.3. Ni marufuku kwa mwanafunzi kujihusisha na vitendo vya wizi, uzinzi, ulevi, uasherati, usagaji, madawa ya kulevya n.k. mwanafunzi akihusika na kosa lolote kati ya hayo **atafukuzwa shule mara moja**.

4.4. Mwanafunzi anatakiwa kuongea lugha ya kiingereza muda wote anapokuwa ndani ya eneo la shule. Mwanafunzi haruhusiwi kuongea na mwalimu au mwanafunzi mwingine kwa lugha nyingine mbali na kiingereza.

4.5. Mwanafunzi anapaswa kuwa na bidii na kufaulu mitihani yake yote ya ndani na nje. Mwanafunzi mvivu atakayeshindwa kufaulu mitihani, **HATAVUMILIWA** na atatakiwa kutafutiwa shule nyingine.

4.6. Mwanafunzi haruhusiwi kuwa nje ya eneo la shule bila ruhusa. Ikiwa mwanafunzi atakuwa na ruhusa ya kuwa/kwenda nje ya shule, mwanafunzi atatakiwa kuvaa sare ya shule na kuwa na kibali kilichosainiwa na walimu husika. Aidha mwanafunzi anapaswa kuzingatia muda wa kurudi shuleni kama ruhusa yake itakavyokuwa inaeleza.

4.7. Mwanafunzi anapaswa kuzingatia kanuni za usafi wakati wote. Ni marufuku kuchora au kukwangua kuta za majengo, viti, meza na madawati au kuvunja/kuharibu vifaa vya maabara au kufanya uharibifu wa mali yoyote ya shule au ya mtu mwingine. Gharama za matengenezo/marekebisho ya uharibifu uliosababishwa na mwanafunzi kwa uzembe zitakuwa juu ya mwanafunzi husika na mzazi/mlezi wake.

4.8. Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na vifuatavyo shuleni: simu, chaja (charger) ya simu, earphone, radio, camera, laini ya simu, (SIM card), smart watch, flash discs, memory cards, compact discs (CD), USB cable, majarida yasiyoendana na maadili ya kitanzania, hereni, mikufu, marashi, ina (rangi ya kucha), kisu, kiberiti au nguo zozote za nje zisizoorodheshwa kwenye mahitaji.

4.9. Mwanafunzi haruhusiwi kuwasha moto bwenini, darasani au mahali pengine popote isipokuwa wakati wa kuchoma taka na kwa maelekezo ya mwalimu.

4.10. Mwanafunzi haruhusiwi kuongea na mgeni yoyote bila ruhusa ya mwalimu husika. Ikiwa amekutana na mgeni shuleni, mwanafunzi amsalimie mgeni kisha amwelekeze ofisini hata kama ni mzazi au jamaa yake.

4.11. Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa sketi/gauni fupi isiyofunika magoti, asiwe na nywele ndefu na kucha ndefu.Vivyo hivyo kwa wavulana hawaruhusiwi kuvaa suruali fupi na nyembamba (modal). Mwanafunzi haruhusiwi kupaka rangi kucha, kung'arisha midomo, au kutumia vipodozi hatarishi vinavyobadili rangi ya ngozi asilia.

4.12. Ni marufuku kwa mwanafunzi kugomea adhabu halali.

4.13. Mwanafunzi anapaswa kutunza mazingira kwa kutotupa taka ovyo na kufanya usafi katika maeneo ya shule atakayopangiwa.

4.14. Mwanafunzi anapaswa kutoa taarifa haraka iwezekanavyo ikiwa ameona au amesikia jambo lolote ambalo ni kinyume na sheria na taratibu za shule. **Ikithibitika kuwa, mwanafunzi alikuwa na taarifa ya kosa au uovu/uharibifu wowote uliotendeka na akashindwa kutoa taarifa hiyo kwa mwalimu husika, mwanafunzi huyo atahesabika kuwa ameshiriki kosa/uovu/uharibifu huo na atachukuliwa hatua sawa sawa na alietenda kosa hilo.**

## 5.0. HALI YA AFYA YA MWANAFUNZI

Ni lazima mzazi/mlezi ahakikishe mtoto wake amefanyiwa vipimo muhimu kabla ya kuja shuleni ili kujua hali yake kiafya. Ieleweke kuwa hali ya afya ya mwanafunzi haiwezi kumzuia kupokelewa shuleni. **Ni muhimu na ni lazima** kujua afya ya mwanafunzi ili kuona namna nzuri ya kuishi nae bila kumuumiza zaidi. Kwa hiyo, ikiwa mwanafunzi ana tatizo maalum la kiafya kama vile asthma, matatizo ya moyo, sickle cell, anaemia, mtatizo ya mifupa, uoni hafifu, kifafa, vidonda vya tumbo, matatizo ya misuli n.k; **taarifa sahihi** iwasilishwe shuleni na mzazi/mlezi. Ikigundulika kuwa mwanafunzi ana tatizo la muda mrefu na mzazi/mlezi anafahamu lakini hakutoa taarifa shuleni, shule **haitawajibika kwa lolote** litakalotokea na mwanafunzi huyo **atafutiwa usajili. Aidha fomu ya medical examination"** ijazwe kwa usahihi kisha irudishwe shuleni.

**6.0. KUHUSU MATIBABU**

Shule itawajibika kupeleka wanafunzi wagonjwa kwenye vipimo na matibabu katika zahanati/hospitali iliyokaribu. Mzazi/mlezi atatakiwa kurejesha gharama zote za matibabu baadae. Aidha wanafunzi wenye kadi za bima ya afya za **NHIF, wanatakiwa kuja na kadi zao za BIMA hiyo.** Endapo mwanafunzi mgonjwa atahitajika kwenda hospitali kubwa/ya rufaa, mzazi/mlezi wake atataarifiwa na atapaswa kuwajibika mara moja.

**7.0. KUTEMBELEA MWANAFUNZI SHULENI**

Wazazi/walezi watatembelea wanafunzi shuleni angalau mara moja kwa kila nusu muhula, yaani angalau mara nne kwa mwaka. Wazazi/walezi watapewa taarifa ya visiting day angalao wiki mbili kabla. Ni muhimu kuzingatia kuwa ratiba hii inaweza kubadilika kutokana na sababu mbalimbali kama vile likizo, mitihani, maelekezo ya serikali n.k.

Wageni/walezi hawaruhusiwi kuja shuleni usiku (yaani baada ya saa kumi na mbili jioni) isipokuwa kwa ruhusa maalum. Ikiwa kuna dharura au uhitaji, mzazi/mlezi anayewajibika kwa mtoto, yaani alieandikishwa shuleni kama namba 1, anaweza kuja kumuona mtoto wake SIKU YOYOTE ili mradi asiingilie ratiba ya masomo darasani au ibada na asije usiku.

**8.0. VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU**

8.1. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

8.2. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

8.3. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

8.4. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

| S/N | JINA | UHUSIANO | PICHA | SIMU |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |

## 9.0 HITIMISHO

Wazazi tunaomba sana tuwe na malezi ya pamoja ili watoto wetu waendelee na wapate kile walichokifuata hapa Shuleni NASSA, yaani ELIMU. Msisitizo wa Bodi ya Shule ni kwamba kila mwanafunzi anatakiwa kusoma kwa bidii na kufaulu kwa kiwango cha alama **65%** au zaidi katika kila somo. Sheria zote za shule zinalenga katika kumfanya mtoto apate mazingira bora ya kujisomea na hatimaye aweze kufaulu vizuri masomo yake.

**TUNATEGEMEA SANA USHIRIKIANO WENU ILI TUTENGENEZA KWA PAMOJA KESHO YA WATOTO WETU.**

**KARIBU SANA NASSA SEKONDARI**

**………………………**
**JAPHET SIRIKWA JOSEPH**
**MKUU WA SHULE**
**SHULE YA SEKONDARI NASSA**

**Muhuri wa Mkuu wa Shule ……………………………….**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule …….............0753 541 548**
- **Makamu Mkuu wa Shule …0765 980 196**
- **Mwandamizi Taaluma … …0766 029 634**
- **Mwandamizi Malezi ………..0683 751 540**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA**

**SHULE YA SEKONDARI YA NASSA**

**FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NASSA**

**1. SEHEMU YA MWANAFUNZI**

Mimi**...........................................................................**ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha tano mwaka…………….katika shule ya sekondari NASSA na nitafika shuleni bila kuchelewa. Ninaahidi kwamba nitatii na kuzingatia sheria zote za shule na za nchi.Pia nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za elimu ya kujitegemea.

Anuani yangu ya kudumu ni:…………………………………………

…………………………………………

…………………………………………

Sahihi ya Mwanafunzi……………………………

2. **SEHEMU YA MZAZI/MLEZI**

Mimi**.......................................................**ninakubali mtoto wangu**………………………………**

Kuchukua nafasi kuingia shule ya Sekondari NASSA. Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na Shule ya Sekondari NASSA na atafika shuleni kwa tarehe iliyopangwa kila wakati. Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na UONGOZI WA SHULE wakati wote na kuhakikisha mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na kwa Taifa.

Anuani yangu ya kudumu ni:…………………………………………

…………………………………………

………………………………………

Namba ya simu …………………………………………

Sahihi ya Mzazi........................................................

Iwapo nitahamishwa au kubadili makazi , ni lazima nitaujulisha uongozi wa shule kwa maandishi

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA**
**SHULE YA SEKONDARI NASSA**
**SIMU NA: 0753 541 548 P.O BOX 440-BUSEGA**
**BARUA PEPE: nassasecondary@gmail.com**

**Ref. No. NASS/……………………….**

The Medical Officer
……………………………………..
……………………………………..
……………………………………..
Please examine ………………………………………………..as to her fitness for pursuing Advanced Level Secondary Education at this School

1. Hemoglobin………………………………………………………………………….
2. P.V Bleeding………………………………………………………………………….
3. i. Sight…………………………………………………………………………...

ii. Hearing…………………………………………………………………………….
4. Blood Pressure………………………………………………………………...
5. Sickle Cell Test………………………………………………………………….
6. Deformity…………………………………………………………………………
7. Urine for Sugar and Pregnancy Test…………………………………………….
8. Epilepsy…………………………………………………………………………
9. Leprosy………………………………………………………………………….
10. Heart examination …………………………………………………………
11. Tumors-breast……………………………………………………………………
12. Pulmonary tuberculosis………………………………………………………….
13. Stool for routine examination……………………………………………………
14. Asthma………………………………………………………………………..
15. Skin diseases……………………………………………………………………

**Comments………………………………………………………………………… ………**

NAME…………………………….SIGNATURE………….... DESIGNATION………………

STATION……………………OFFICIAL STAMP……………………. DATE…………………